

# Mafunzo kwa Urais wa Akidi ya Ukuhani wa Haruni na Urais wa Darasa la Wasichana



### KUITWA NA MUNGU

- Je, inamaanisha nini kwangu kuitwa na Mungu?



### WATUMIKIE WALE UNAOWAHUDUMIA

- Je, ni kwa jinsi gani nitaweza kuwajua na kuwapenda washiriki wote wa akidi yangu au darasa langu?
  **JIFUNZE ZAIDI:** Karani wa kata anaweza kutoa orodha ya washiriki wa akidi au wa darasa.
- Je, ni kwa jinsi gani nitafuata mfano wa Mwokozi wa kuhudumia?



### MAJUKUMU YA KIUTAWALA

- Je , ni mikutano gani ninayohudhuria na kupanga?
  **JIFUNZE ZAIDI KUHUSU:** mikutano ya urais wa akidi au darasa na mabaraza ya vijana ya kata kama nyongeza ya mikutano na shughuli za kawaida za Kanisa (Ona *Kitabu cha Maelezo ya Jumla: Kuhudumu katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho*, 10.4.3, 10.4.4, 11.3.4.3, 11.3.4.4, 29.2.9, ChurchofJesusChrist.org).
- Je, ni majukumu gani ya kiutawala niliyonayo? Je, ni nyenzo zipi zinaweza kunisaidia?
  **JIFUNZE ZAIDI KUHUSU:** ajenda za mikutano (ona "Mfano wa Ajenda ya Mkutano wa Urais"), kuendesha mikutano, kugawa majukumu, kufuatilia majukumu, na kuwasalimia washiriki wa akidi au darasa (ona *Kitabu cha Maelezo ya Jumla,* sura ya 4).



### PANGA MIKUTANO NA SHUGHULI

- Je, ni kwa jinsi gani tutakuwa na mikutano yenye kuinua na ya kiroho ya Jumapili? (Ona *Njoo, Unifuate—Kwa Ajili ya Akidi za Ukuhani wa Haruni na Madarasa ya Wasichana*.)
  **JIFUNZE ZAIDI KWENYE:** ComeFollowMe.ChurchofJesusChrist.org.
- Je, ni kwa jinsi gani tutakuwa na huduma na shughuli zinazoshirikisha na zilizosheheni matokeo? (Ona "Miongozo ya Huduma na Shughuli kwa Vijana.")
  **JIFUNZE ZAIDI KWENYE:** ChildrenandYouth.ChurchofJesusChrist.org.

# Taarifa kwa ajili ya Uaskofu na Viongozi wa Wavulana na Wasichana Wakubwa

Uaskofu unalo jukumu la kutoa mafunzo kwa urais mpya ulioitwa wa akidi ya Ukuhani wa Haruni na urais wa darasa la Wasichana. Utoaji mafunzo kwa urais ni hatua muhimu katika kuwasaidia viongozi wa vijana kufanikiwa katika miito yao.

Nyenzo zifuatazo ni mapendekezo ya kuwasaidia washiriki wa uaskofu pale wanapoufunza urais mpya au wanapoufundisha urais uliopo. Nyenzo hizi na maswali ya awali vingeweza kutumiwa ili kuongoza mjadala mfupi wa kufunza au kufundisha urais mpya au uliopo katika mabaraza ya kata ya vijana au katika mazingira mengine. Kama itakavyoelekezwa na uaskofu, viongozi wa Wavulana na Wasichana wangeweza pia kurejelea nyenzo hizi katika mkutano wa urais wa akidi au wa darasa.

## NYENZO ZA MAFUNZO

### **Kuitwa na Mungu** DAKIKA 8–10

*"Ili kuwa viongozi wa Kanisa wanaofaa, lazima tujifunze somo hili muhimu: uongozi katika Kanisa haulengi zaidi katika kuongoza wengine kama ilivyo kuhusu utayari wetu wa kuongozwa na Mungu" (Dieter F. Uchtdorf, "Aliye Mkuu kati Yenu,"* Ensign *or* Liahona, *Mei 2017, 80).*

- Urais wa akidi na wa darasa unaitwa kwa ufunuo (ona Yohana 15:16).
- Urais wa akidi ya Ukuhani wa Haruni unafanya kazi kwa funguo zilizotolewa wakati marais wa akidi wanapotawazwa. Urais wa darasa la Wasichana hufanya kazi kwa mamlaka ya ukuhani iliyopokelewa wakati urais unapotawazwa (ona Mafundisho na Maagano 42:11; 107:5; Makala ya Imani 1:5; Kitabu cha Maelezo ya Jumla, 3.4.1).
- Urais unawajibika kwa Bwana na kwa viongozi Wake (ona Mafundisho na Maagano 104:11–13; *Kitabu cha Maelezo ya Jumla,* 4.2.6).
- Urais unahudumu kama mfano kwa ajili ya washiriki wa akidi au wa darasa (ona 1 Timotheo 4:12; Alma 17:2–3).

### **Wahudumie Wale Unaowatumikia** DAKIKA 5–8

*"Umeitwa ili kumwakilisha Mwokozi. . . . Mikono yako ya kuinua [inakuwa] sawa na mikono Yake" (Henry B. Eyring, "Inuka kwenye Wito Wako,"* Ensign *au* Liahona, *Nov. 2002, 76).*

- Wahesabu, chukua majina, na walishe neno la Mungu wale unaowahudumia (ona Moroni 6:4).
- Wasaidie wengine kumfuata Mwokozi (ona *Kitabu cha Maelezo ya Jumla,* 4.2.3).

### **Majukumu ya Kiutawala** DAKIKA 5–8

*"Huu ni muujiza wa mabaraza ya Kanisa: kusikilizana na kumsikiliza Roho!" (M. Russell Ballard, "Counseling with Our Councils,"* Ensign, *May 1994, 26).*

- Shiriki katika mabaraza ya vijana ya kata (ona *Kitabu cha Maelezo ya Jumla,* 29.2.9).
- Fanya mikutano ya akidi au darasa ya mara kwa mara (ona *Kitabu cha Maelezo ya Jumla,* 10.4.3, 11.3.4.3; "Mfano wa Ajenda ya Mkutano wa Urais").
- Kuza ujuzi wa uongozi ili kukamilisha kazi (ona *Kitabu cha Maelezo ya Jumla,* 4.2).

### **Panga Mikutano na Shughuli** DAKIKA 5–8

*"Kila shughuli, kila somo, vyote tunavyofanya Kanisani, vinaelekeza kwa Bwana na nyumba Yake takatifu" (Russell M. Nelson, "Personal Preparation for Temple Blessings,"* Ensign, *May 2001, 32).*

- Jifunze majukumu yako (ona *Kitabu cha Maelezo ya Jumla,* Sura za 10–11).
- Panga na ongoza kama unavyoelekezwa na Roho (ona Mafundisho na Maagano 43:8–9; 88:119; Moroni 6:9).

## MAELEKEZO YA ZIADA

Fursa za kukuza ujuzi wa uongozi zinaendelea katika mikutano ya baraza la vijana ya kata na mikutano ya kawaida ya urais. Kwa ajili ya nyenzo za kusaidia katika juhudi hii, ona Nyenzo za Urais wa Akidi na wa Darasa.

KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO

© 2019 by Intellectual Reserve, Inc. All rights reserved. 8/19. Tafsiri ya *Quorum and Class Presidency Orientation v2.* Swahili. PD60009511 743. Kimepigwa chapa Marekani